



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SCHOOL INFORMATION SYSTEM (SIS)

STUDENT PORTAL

MWONGOZO WA MWANAFUNZI

UJAZAJI WA FOMU YA MACHAGUO
YA MWANAFUNZI (SELF FORM)



OKTOBA 2026

MWONGOZO WA MWANAFUNZI

1 Utangulizi

Mwongozo huu umeandaliwa kumsaidia Mwanafunzi kutumia Student Portal katika ujazaji wa SELFORM ya mwanafunzi wa Kidato cha Nne. Mwongozo unaelekeza hatua zinazopaswa kufuatwa na mwanafunzi wakati wa ujazaji.

2 Jinsi ya Kuingia

Andaa **Namba Yako ya PREM** na **Jina Lako la Kati** kama zilivyosajiliwa kwenye mfumo wa SIS. Taarifa hizi lazima zilingane na kumbukumbu zilizopo kwenye mfumo wa SIS.

Kwenye kivinjari (web browser) ingiza <https://sis.tamisemi.go.tz>

3 Chagua aina ya akaunti

- i. Bonyeza **Create account (Student/Parent)**.
- ii. Chagua **Student**, kisha **Continue**

4 Thibitisha taarifa na tengeneza nenosiri

- i. Jaza **Namba** ya **PREM** na **Jina la Kati** kama zilivyo kwenye mfumo wa SIS.
- ii. Bonyeza **CONFIRM DETAILS**,
- iii. kisha fuata hatua za mfumo kutengeneza nenosiri lako (password). Liweke kuwa siri.
- iv. Utakua umetengeneza akaunti yako

5 Ingia Kwenye Mfumo

- i. Kwenye sehemu ya kuingia kwenye mfumo weka **Namba yako PREM**.
- ii. Kwenye namba ya siri, weka **Nenosiri** ulilotengeneza
- iii. kisha bonyeza **LOGIN**.

Ikiwa hautofanikiwa kuunda akaunti au kuingia kwenye mfumo, wasiliana na Mkuu wa Shule ili kuhakiki taarifa zako kwenye mfumo wa SIS.

KUJAZA NA KUTUMA SELFFORM

6 Fungua Selfform

Baada ya kuingia kwenye mfumo, utaona menyu inayoonyesha **Dashboard, My details, Selection profile Academics** na **Selfform**. Bonyeza **Selfform** kufungua fomu ya uchaguzi. Fomu itafunguka ikionyesha maeneo yafuatayo;

- i. Particulars - taarifa binafsi
- ii. Choice – Machaguo (Pathways)
- iii. Details – taarifa za ziada
- iv. Declaration
- v. Review

6.1. Hatua ya kwanza - Particulars (Taarifa Binafsi)

Eneo hili linaonyesha taarifa za mwanafunzi. Kagua taarifa hizo kuhakikisha usahihi wake. Ikiwa kuna mapungufu kwenye taarifa za mwanafunzi, mfumo unakuruhusu kurekebisha maeneo yafuatayo;

- i. Jinsi
- ii. Tarehe ya kuzaliwa
- iii. Namba ya simu ya mzazi au mlezi
- iv. Halmashauri ya anakoishi mwanafunzi (Home Council)
- v. Barua pepe
- vi. Hali ya ulemavu (Kama ipo)

Ikiwa kuna taarifa nyingine zenye mapungufu wasiliana na Mkuu wa shule kwa msaada zaidi.

6.2. Hatua ya Pili - Choices (Machaguo)

Eneo hili linamuwesha Mwanafunzi kupanga machaguo (Academic Choice) kwa kuzipa vipaumbele kuanzia kipaumbele cha **I hadi 5**, ambapo kipaumbele cha **I** kinawakilisha chaguo la kwanza kwa umuhimu. Hakikisha njia zote tano za masomo zimepewa kipaumbele.

KUJAZA NA KUTUMA SELF FORM

6.3. Hatua ya tatu - Details (Taarifa za Kina)

Eneo hili linamwezesha Mwanafunzi kufanya machaguo ya kina (Detailed Choices) kwa kila kundi la machaguo lililopangiwa kipaumbele kwa kuchagua tahasusi au kozi anazopendelea pamoja na shule au vyo vinavyotoa tahasusi au kozi hizo. Machaguo hayo yanapaswa kupangwa kwa kuzingatia vipaumbele na masharti yaliyowekwa kwenye mfumo.

6.4. Hatua ya Nne - Declaration (Tamko)

Soma na thibitisha usahihi wa taarifa za machaguo yaliyojazwa, kisha kubali tamko kwa kufuata maelekezo ya mfumo.

6.5. Review - Kagua na uwasilishe

Kagua usahihi wa taarifa na mpangilio wa machaguo yote yaliyojazwa. Ukiridhika, bofya kitufe cha kuwasilisha machaguo kwa Mkuu wa Shule kwa ajili ya uhakiki na uthibitisho. Hakikisha hali ya machaguo imebadilika kutoka **Draft** kuwa **Awaiting Verification**.

7.0. Uwasilishaji wa Maoni, Maswali na Mapendekezo

Huduma hii ya kujaza machaguo ni bure na endapo wanafunzi watapata changamoto, wawasiliane na Dawati la Huduma la Mteja kupitia barua pepe: helpdesk@tamisemi.go.tz au kuwasiliana moja kwa moja na Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa simu **+255 262 160 210** na **+255 735 160 210**. Aidha, pamoja na maelekezo hayo, kwa mwanafunzi, mzazi/mlezi atakayekuwa na suala linalohitaji maelezo au ufafanuzi zaidi aende katika Ofisi za Elimu za Mikoa na Halmashauri.